Toleo 86 - Shaaban 1445 H / Machi 2024 M

# Jarida la UQAB




## Miaka 103 (H)

# BADO TUKO MAYATIMA!

uqab.info
uqab_htk
UQABMagazine

Afisi ya Habari Afisi kuu ya Habari

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

KUMB: 22/1445 | Jumatano, 12 Rajab 1445 H | 24/01/2024 M


**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Serikali ya Rishi Sunak Yaipiga Marufuku Hizb ut Tahrir na Kuisingizia Uongo, Kuibandika Upanga wa “Kuchukia Mayahudi” dhidi ya wale Wanaopinga Mauaji Yanayofanywa na umbile la Kiyahudi huko Gaza

Alhamisi iliyopita, Januari 18, 2024, serikali ya Uingereza ilipigia kura Bungeni ombi la kupiga marufuku Hizb ut Tahrir, ambapo marufuku hiyo iliidhinishwa na wabunge wachache waliokuwepo kwenye kikao hicho. Hii ni baada ya kutekeleza kile kilichoitwa kwa uwongo mjadala wa azimio lililopendekezwa, wakati uhalisia ni mkusanyiko wa hotuba za kisiasa za kuhadaa rai jumla, ili kutoa kibali kwa umbile la Kiyahudi kuendelea na mauaji yake ya kila siku dhidi ya watu wa Palestina, na kubandika upanga wa "chuki dhidi ya Mayahudi" dhidi ya rai jumla ili isionyeshe au kutaka upinzani dhidi ya uvamizi huo.

Kwa hivyo, kwa urahisi kabisa, hizb imepigwa marufuku baada ya kufanya kazi kwa uwazi nchini Uingereza katika miongo minne yote, kwani haikurekodiwa kwamba ilifanya vitendo vyovyote vya kisilaha nchini Uingereza au popote duniani katika kipindi hiki. Na wale waliokuwa na upendeleo dhidi yake, hawakuweza kuthibitisha uwongo wao na kashfa kwamba Hizb ut Tahrir ina uhusiano wowote na ugaidi. Na leo hii hapa, serikali ya Rishi Sunak na kisingizio kibaya, kwamba Hizb ni shirika la kigaidi kwa sababu ya msimamo wake juu ya vita vya Gaza!

Waziri wa Usalama wa Rishi Sunak hakuweza kuwasilisha katika kikao hicho ushahidi halisi wa kuwepo kwa vitendo vya kigaidi, bali alichosema ni kwamba Hizb iliyataka majeshi ya Kiislamu kunyanyuka na kupigana na jeshi la umbile la Kiyahudi. Ama kuhusu “ushahidi” wake uliosalia, si chochote ila ni rekodi ile ile iliyovunjwa ya utetezi wa Wazayuni nchini Uingereza, ambao ulimpatia ripoti zinazozungumzia hofu ya Mayahudi wa Uingereza kuhusiana na maandamano ya Wapalestina! Huu ndio “ushahidi” wake, wakati mazungumzo yake mengine yote yalikuwa hotuba ya kisiasa yenye kashfa za uwongo kuhusu Hizb kuwa na chuki dhidi ya Mayahudi, na simulizi mpya ya matukio kama alivyopewa na umbile la Kiyahudi. Kwao, historia ilianza asubuhi ya tarehe 7 Oktoba 2023, kana kwamba mzozo na uvamizi wa ardhi ya Palestina haukuwepo kabla ya siku hiyo! Pia walirudia madai ya vyombo vya habari vya Kiyahudi kuhusu mauaji ya watoto na ubakaji wa wanawake, wakati ripoti na ushuhuda wa video wa kukiri kwa askari wa uvamizi na walowezi unathibitisha kwamba walipewa amri ya kupiga mabomu makaazi na kila mtu ndani yake. Polisi wa eneo hilo pia hawakuweza kupata waathiriwa wa madai ya ubakaji. Inatosha kukumbuka kashfa ambayo Rais Joe Biden wa Marekani aliingia ndani yake wakati alipowasilisha uwongo wa umbile la Kiyahudi kuhusu kukatwa vichwa kwa watoto, na kisha ikatokea kwamba walimdanganya yeye na ulimwengu.

Ujasiri wa Waziri wa Usalama wa Rishi Sunak katika kupotosha rai jumla unaonyeshwa pale alipopuuza kauli na matendo ya wanasiasa wa umbile la Kiyahudi ambayo yaliripotiwa na vyombo vya habari vya kimataifa na kuchapishwa kwenye magazeti, na ambayo kwa hakika yanahitaji kupigwa marufuku na kuadhibiwa, ikiwa ni pamoja na:

•Kauli ya Benjamin Netanyahu, ambaye alisema: "Tutaigeuza Gaza kuwa kisiwa kisicho na watu."

•Netanyahu pia alinukuu simulizi ya Kiyahudi inayosema: “Sasa nendeni mkaangamize kila walivyo navyo, wala msimuache mwanamume, mwanamke, mtoto, wala watoto wachanga, wala ng’ombe, wala kondoo, wala ngamia, wala punda.

***Endelea... UK 3***

•Kauli ya Waziri wa Turathi Amihai Eliyahu kuangusha bomu la nyuklia mjini Gaza.

•Kauli ya Waziri wa Fedha Bezalel Smotrich, ambaye alitoa wito wa kufukuzwa nchi watu wa Gaza.

•Taarifa ya Waziri wa Usalama wa Kitaifa katika umbile la Kiyahudi, Itamar Ben-Gvir, kwamba kitu pekee kitakachoingia Gaza ni mamia ya tani za vilipuzi ambavyo vitaangushwa na jeshi la anga.

•Kauli ya Waziri wa Ulinzi Yoav Gallant, ambaye alisema: "Tunapigana na wanyama huko Gaza."

•Taarifa ya msemaji wa jeshi la umbile la Kiyahudi, Daniel Hagari, kwamba lengo ni uharibifu, sio kutengeza.

•Taarifa ya rais wa umbile hilo, Isaac Herzog, kwamba kuzungumza juu ya kutowajibika kwa raia sio sahihi.

•Kauli ya mwanachama wa Knesset Merav Ben Ari kwamba "watoto wa Gaza ndio waliojiletea haya wenyewe."

•Kauli ya balozi wa zamani wa umbile la Kiyahudi katika Umoja wa Mataifa, Dan Gillerman, kwamba watu wa Palestina ni wanyama wa kutisha, wasio na ubinadamu.

•Kauli ya mtafiti na mwanahabari maarufu Mordechai Kadar kwamba kufananishwa kwa Wapalestina na wanyama ni tusi kwa wanyama.

Mbali na matamshi ya waandishi wa habari wa Kizayuni, wataalamu wa vyombo vya habari, na watafiti walioandaliwa na idhaa zenye uhusiano na umbile la Kiyahudi, wanaochochea uharibifu kamili wa Gaza.

Labda nia ya Waziri wa Usalama ya kuwa Waziri Mkuu badala ya Sunak (kama alivyosema mara kwa mara) ilimfanya afumbie macho kauli hizi za wanasiasa wa umbile la Kiyahudi, na badala yake kuwa na shauku ya kutoa marufuku ya Hizb ut Tahrir kama kafara kwa utetezi wa wa Wazayuni, ambao unaonekana kulegea kwenye korido za Ikulu ya Westminster, ili pengine atapata upendeleo wao wakati ujao.

Kwa upande wa wasemaji wengine waliohudhuria kikao hicho, mazungumzo yao hayakuwa zaidi ya kurushiana maneno ya kisiasa wenyewe kwa wenyewe, kwani hawakupinga madai yoyote ya Waziri wa Usalama, bali waliongeza kwenye uongo wake uongo mkubwa zaidi, kama wengine wao kusema kwamba Hizb ut Tahrir inapata msaada kutoka Iran! Na wanaosema kuwa kuua na kuwaangamiza Mayahudi ndio kipaumbele cha hizb! Mbali na kukanusha kwao kuwa hizb inapeperusha sauti ya mateso ya watu wa Palestina kwa Waislamu wa Uingereza!
Pia wazungumzaji hawakusita kueleza kutoridhishwa kwao na kuona maandamano ya kuwaunga mkono watu wa Palestina, na hawakusita kuyataja kuwa ni "mabaya" na kuwaelezea wale wanaoyahudhuria kuwa "sehemu mbaya zaidi za jamii." Walikariri propaganda za Wazayuni kwamba ni dhihirisho la chuki dhidi ya Mayahudi, huku uhalisia ni maandamano dhidi ya umbile la Kiyahudi linaoikalia kwa mabavu Palestina, jambo ambalo Hizb ut Tahrir nchini Uingereza ilieleza waziwazi katika taarifa zake zilizotangulia. Lakini upendeleo wa wazungumzaji juu ya umbile la Kiyahudi uko wazi mithili ya mchana ambapo baadhi yao walitangaza kwamba wameshiriki katika maandamano "dhidi ya chuki dhidi ya Mayahudi," ambayo kwa kweli yalikuwa maandamano ya kuegemea na kuunga mkono umbile la Kiyahudi, ambapo bendera za umbile la Kiyahudi zilinyanyuliwa kuanzia mwanzo hadi mwisho, na kauli mbiu, maoni na rai za waliohudhuria kwa kiasi kikubwa zilihusu vita vinavyoendelea Palestina, kama ilivyokuwa wazi katika mahojiano ambayo yaliripotiwa kutoka ndani ya maandamano.

Hii ni sera ya unafiki. Wakati jeshi la umbile la Kiyahudi liliposhambulia kwa mabomu Hospitali ya Baptist mjini Gaza na kuua zaidi ya wahasiriwa 500 waliokuwa kwenye ua wa hospitali hiyo, Rishi Sunak alitilia shaka chanzo cha kombora lililoipiga hospitali hiyo, na hiyo ni kwa sababu umbile la Kiyahudi lilitaka kukwepa jukumu la kulipua mabomu hospitali hiyo. Lakini wakati jeshi la umbile la Kiyahudi lilipozishambulia kwa mabomu hospitali zote za Gaza, shule, sehemu za kuoka mikate, misikiti na makanisa, na kuwalipua wahamiaji walipokuwa wakihamia kati ya miji yake, wakikata maji na umeme kutoka kwao, na hawakusita kuyachukua na kuhalalisha vitendo hivi vyote, Rishi Sunak hakuona tena kwamba ukatili huu ulistahiki umakinifu wake!

Inaonekana kwamba wanasiasa wa serikali ya sasa ya Uingereza ni Wazayuni kabisa. Hata "kamishna wa serikali wa kupambana na misimamo mikali," ambaye Waziri wa Usalama alimshukuru kwa ushauri aliotoa kuhusu kupiga marufuku Hizb, ana upendeleo wa wazi dhidi ya Waislamu. Alichaguliwa kwa uangalifu katika nafasi hii, kwani ana historia ya kufanya kazi katika taasisi zinazochukia sana Waislamu, kama zile zinazohusishwa kwa karibu na Rais wa zamani wa Marekani, Donald Trump. Waislamu hawajasahau marufuku ya kusafiri ambayo Trump aliweka kwa Waislamu wanaokuja Marekani. Mbali na vituo vingine vya utafiti, kamishna wa serikali aliingilia kati kabla ya

***Endelea... UK 4***

kuchukua wadhifa wake. Taasisi hizi ambazo zimezama kutoka kichwa hadi miguu katika uchochezi dhidi ya fikra za Uislamu, dhidi ya wahamiaji wa Kiislamu, na dhidi ya wanaharakati wa Kiislamu. Badala yake, chuki ya kamishna huyu wa serikali imefikia hatua kwamba anachukulia neno "Uislamu" sawa na neno "msimamo mkali," kama alivyosema katika moja ya makala yake ya Heritage Foundation. Je vipi jukumu la wadhifa kama huo litapewa mtu mwenye siasa na upendeleo dhidi ya Uislamu na Waislamu namna hii?!

Hii ndio serikali ya Rishi Sunak na wanasiasa wake walioamua kupiga marufuku Hizb ut Tahrir; Wamebeba chuki iliyojificha, na ni ala za ajenda ya Wazayuni, inayowataka Waislamu wa Uingereza kusimama pembeni na kutazama mauaji na njaa ya ndugu zao huko Gaza na wasikasirikie hilo wala kuyataka majeshi ya Kiislamu yahamasike kuwanusuru. Serikali ya Rishi Sunak inawataka Waislamu sio tu kutokuwa na hisia za Uislamu, bali inawataka wasiwe na hisia kabisa ili kusibakie chochote katika ubinadamu wao!

Ni wazi kuwa serikali ya Rishi Sunak inavaa vazi la Chama cha Conservative, wakati uhalisia ni kundi la mrengo wa kulia uliokithiri sawa na wahafidhina ambao walichukua madaraka nchini Marekani mnamo 2001 na kutangaza kampeni maarufu ya "Vita dhidi ya Ugaidi", ambapo mamilioni ya Waislamu waliuawa. Tukumbuke kwamba moja ya vipengee muhimu vya kampeni hiyo ilikuwa ni sera ya kuwatia hofu Waislamu wa nchi za Magharibi kutokana na kupinga Marekani na washirika wake kuua ndugu zao katika nchi za Kiislamu. Huu ndio mtazamo wa serikali ya Rishi Sunak kwa Waislamu nchini Uingereza hivi leo. Inataka waangalie mauaji ya watoto na wanawake wa kaka/dada zao huko Palestina na wakae kimya wasifanye lolote! Inataka kuwafanya Waislamu wa Uingereza kuwa miili inayotembea bila roho, kwa kutumia mantiki ile ile aliyoieleza George Bush Mwana alipouambia ulimwengu, “Wewe ima uko pamoja na sisi au uko pamoja na magaidi,” kwa hiyo kila Muislamu amekuwa gaidi kwao mpaka aseme wanachokisema!

Serikali ya Rishi Sunak imeshindwa kukabiliana na hoja kwa hoja na kutoa ushahidi wa kashfa yake, na kwa hivyo itashindwa mbele ya rai jumla. Imeileta jamii katika hatua ya ukandamizaji wa kifikra, na imezindua taasisi za serikali bila kujua kuamiliana na jamii kwa msingi huu. Vitendo kama hivyo ambavyo vinapingana waziwazi na ufisadi, humomonyoa ari ya jamii na kuua nguvu yao. Kila mtu anaona mauaji yanayofanyika dhidi ya watu wa Palestina, na kila mtu anaona kwamba kile serikali ilichokifanya ni kujaribu kuinyamazisha Hizb isifichue uhalifu huo, na kuwatia hofu Waislamu kutokana na ufikiriaji wa pamoja. Ni kana kwamba serikali ya Sunak inasema kitu kama: "Nyinyi Waislamu mmekatazwa kufikiria juu ya masuluhisho yote"! Kila mtu anajua kwamba vitendo vya Hizb katika miongo minne iliyopita vilikuwa vitendo vya kifikra na kisiasa ambavyo havikuwa na uhusiano wowote na ugaidi, na kwa hivyo marufuku hii itaashiria kuingia kwa awamu ya kushambulia rai jumla kila inapopingana na maoni ya mamlaka.

Ulinganizi wa Hizb ut Tahrir uko wazi na rahisi; Mwamko wa Umma wa Kiislamu, umoja wake, na kurudi kwa Khilafah yake kama ilivyokuwa zama za Maswahaba, kwa kauli na vitendo, na hili limekuwa nguzo madhubuti katika moyo wa kila Muislamu anayeupenda Uislamu na kujali maslahi yake. Kwa hivyo, ulinganizi wa Hizb ut Tahrir utabakia, kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu, thabiti, angavu na safi, ukielekea kwenye lengo lake, yote hayo kwa ajili ya kumridhisha Mwenyezi Mungu.

Kwa hivyo kuweni na subira, watu wetu wa Uingereza. Kuweni na Mwenyezi Mungu, Utukufu ni wake, Yeye anakutoshelezeni, na Yeye ni Msaidizi wenu, na kumbukeni kwamba vitendo vyenu vinapaswa kuwa vya ikhlasi kwa ajili Yake, Utukufu ni Wake. Mwenyezi Mungu amewaahidi Waislamu tamkini tena, kama vile tulivyobashiriwa na Mtume wake (saw) na Mwenyezi Mungu hatavunja ahadi yake, basi kuweni wa bishara njema. Ametutajia katika Qur’an Tukufu kuhusu mabadiliko ya hali ya nchi na mataifa. Ametukumbusha kuwa suala zima liko chini ya himaya yake, kabla na baada ya kuinuka na kuanguka kwa nchi.

Mwenyezi Mungu (swt) asema:

**﴿الم * غُلِبَتِ الرُّومُ * فِي أَدْنَى الأَرْضِ وَهُم مِّن بَعْدِ غَلَبِهِمْ سَيَغْلِبُونَ * فِي بِضْعِ سِنِينَ لِلَّهِ الأَمْرُ مِن قَبْلُ وَمِن بَعْدُ وَيَوْمَئِذٍ يَفْرَحُ الْمُؤْمِنُونَ * بِنَصْرِ اللهِ يَنصُرُ مَن يَشَاءُ وَهُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ * وَعْدَ اللهِ لا يُخْلِفُ اللهُ وَعْدَهُ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لا يَعْلَمُونَ * يَعْلَمُونَ ظَاهِراً مِّنَ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَهُمْ عَنِ الآخِرَةِ هُمْ غَافِلُونَ﴾**

**“Alif-Lãm-Mĩm * Warumi wameshindwa, Katika nchi iliyo karibu. Nao baada ya kushindwa kwao watashinda * Katika miaka michache. Amri ni ya Mwenyezi Mungu kabla yake na baada yake. Na siku hiyo Waumini watafurahi. * Kwa nusura ya Mwenyezi Mungu humnusuru amtakaye. Naye ndiye Mwenye nguvu Mwenye kurehemu * Ni ahadi ya Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu havunji ahadi yake. Lakini watu wengi hawajui * Wanajua hali ya dhaahiri ya maisha ya dunia, na wameghafilika na Akhera.” [Ar-Rum 1-7].**

**Mhandisi Salah Eddine Adada**
**Mkurugenzi wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

Afisi ya Habari
Afisi kuu ya Habari

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

KUMB: 23/1445 | Ijumaa, 28 Rajab 1445 H | 09/02/2024 M

**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Tarehe 28 Rajab Mwaka huu ni Ukumbusho Mkubwa kuliko Miaka Yote Iliyopita kwamba Kuregea kwa Khilafah ni Hitajio la Haraka

Kumbukumbu ya kuanguka kwa Khilafah mnamo tarehe 28 Rajab inakuja mwaka huu ikiwa na athari zaidi ya kukumbukwa kuliko miaka iliyotangulia. Inakuja na jeraha la Palestina linalotiririka damu nyingi zaidi kuliko hapo awali, na kutukumbusha kwamba suala la kupotea kwa Palestina lilikuwa na bado lina uhusiano wa karibu na kuanguka kwa Khilafah. Tangu ilipovunjwa Khilafah mnamo tarehe 28 Rajab mwaka 1342 H, tangu siku hiyo Palestina imekuwa chini ya ukaliwaji kimabavu wa moja kwa moja wa kikoloni, na hakuna aliyeikomboa kutoka katika nchi zilizoundwa na Sykes na Picot.

Kwa hakika, vita vya Gaza mwaka huu vinanyooshea kidole chake kwa Umma wa Kiislamu, na kuuliza, “Kwa nini humkutunusuru?!”, na Umma wa Kiislamu unajitazama, unashangaa na kuuliza, “Kwa nini hatukuweza kuwanusuru?” Jibu ni kwamba Umma wa Kiislamu hauko huru, bali ni mfungwa wa Sykes-Picot (makubaliano ya mipaka). Uhalisia wa nchi za Kiislamu ni kwamba ni jela kwa watu wao. Ni uhalisia ambao hauwezi kukwepwa, na yeyote anayevuka huingia kwenye mzunguko mchafu ambao hujilisha wenyewe. Mfungwa hawezi kumwachilia huru mfungwa mwingine.

Vita vya Gaza hivi leo ni ushahidi wenye nguvu zaidi kwamba Khilafah ni hitajio la haraka kwa Umma wa Kiislamu, kwani ina uwezo wa kukusanya majeshi ya Waislamu na kuyapeleka mahali yanapopaswa kuwepo. Haijuzu kwake kushindwa kuwanusuru Waislamu. Achilia mbali kwamba ardhi iliyobarikiwa ya Palestina daima imekuwa ikipata ushindi kutoka kwa Waislamu wote. Tangu utume wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw), nyoyo za Waislamu zimeitamani ardhi hii iliyobarikiwa, kwani ni kibla cha kwanza kati ya vibla viwili, ardhi ya Safari ya Usiku na Kupaa mbinguni, ardhi ya Rabat, ardhi ya Ufufuo, uwanja wa vita wa mujahidina, na rekodi bora ya ushindi wa Uislamu.

Kwa hiyo, hivi sasa, wakati wa matatizo, na kwa kumbukumbu hii, kumbukumbu ya kuvunjwa kwa Khilafah, tunauomba Umma wa Kiislamu ufanye kazi ya kusimamisha Khilafah, tukikumbuka ukweli ulio wazi kwamba Palestina ilipeanwa kwa Wazayuni wakati Khilafah ilipovunjwa, na haitaregea isipokuwa kwa kurudi Khilafah. Hii inatosha (sababu) kwa Umma wa Kiislamu kufanya kazi kwa umakini na kwa makusudi ya kuiregesha.

**Kwa Watu Wenye Nguvu na Ulinzi, tunasema:**

**Enyi Wanajeshi katika Majeshi ya Kiislamu,** Umma unakuiteni, basi uungwana wenu uko wapi?! Umekupeni watoto wao kama askari kuwatumia, na ukakununulieni silaha kwa fedha zake, na leo unapiga kelele kwa kinywa kipana: **“Mko wapi, enyi majeshi ya Waislamu?”** Je, mtaunusuru kwa wema na utiifu kwa Dini yenu?

**Enyi Askari katika Majeshi ya Kiislamu,** msingoje amri za kuhamasishwa jeshi zitoke kwa watawala, kwani wamejiingiza ndani ya nyoyo zao usaliti mpaka wakawa ni tafsiri ya uhaini. Msingojee idhini ya Magharibi, kwani inataka kuwaweka ndani ya kambi, ili msisonge isipokuwa inapotaka kuwatumia kuua familia zenu na kuvunja nyumba zenu wenyewe. Bali mtegemeeni Mwenyezi Mungu (swt) pekee, ambaye amewatia nguvu askari Wake, na juu ya Ummah wa Kiislamu ambao umekuwa na bado unakuungeni mkono kwa pesa na uhai.

**Kwa vyombo vya habari, wanamaoni, na wale walio na mimbari, kalamu, na majukwaa... Je, bado mungali hamjaelewa?!**

***Endelea... UK 6***

**Ni kweli mbili zisizoweza kuepukika: Palestina ilipotea wakati Khilafah ilipopotea, na mipaka ya Sykes-Picot ni gereza kubwa lililoundwa kuwafunga Waislamu ...** Kwa hiyo, haijalishi munajaribu sana kiasi gani, haijalishi munatafuta kiasi gani, na haijalishi munajaribu kiasi gani, kweli hizi mbili ni minyororo miwili inayoufunga Ummah wa Kiislamu ardhini na kuzuia mwamko wake. Minyororo hii miwili iliundwa katika korido za mkoloni Kafiri Magharibi, na kwa hiyo munaona kwamba nchi za Magharibi zina nia kubwa ya kuhifadhi mambo haya mawili. Wanasiasa wa Kimagharibi na vyombo vyao vya habari vinakataza kuwasilisha Khilafah kama mfumo wa kisiasa na wanachuki kali na misingi yake, kama vile Sharia, jihad, na maisha ya Kiislamu. Nchi za Magharibi pia zimejiandaa kuwatambua watawala na serikali fisadi zaidi katika nchi za Kiislamu, na kupuuza jinai zao na hata kuwalinda dhidi ya uwajibikaji, mradi tu wahifadhi mipaka ya Sykes-Picot na kazi yake ya kijiografia; ambayo ni kuzikoloni na kuzigawanya nchi za Kiislamu. Kwa hiyo, muna kazi kubwa, ambayo ni kunyanyua ufahamu wa rai jumla katika Umma wa Kiislamu na kurekebisha dira yake kuelekea kufanya kazi ya kuiregesha Khilafah kwa kuwataka watu wa Nusra (msaada wa kimada) wachukue hatua, waondoe nchi kutoka kwa Sykes-Picot, na kusimamisha Khilafah. Kwa hivyo fanyeni hisa yenu na muwakumbushe watu kwamba ardhi iliyobarikiwa ya Palestina ilipotea wakati Khilafah ilipopotea, na kwamba makubaliano ya Sykes-Picot ni gereza kubwa lililoundwa kuwafunga Waislamu.

**Kwa Ummah mzima wa Kiislamu:**

**Enyi Waislamu,** hapana shaka kwamba damu inachemka katika mishipa yenu mnapotazama kuuawa kwa watu wa Gaza na kutelekezwa kwao na watawala. Hili ni makusudi, kwani wanataka kukufanyeni mujisikie wanyonge ili mufikiri hakuna suluhisho. Lakini ukweli ni kwamba suluhisho lipo, na linaanza na wito wenu mliouita wakati huu, ambao ni, **“Mko wapi enyi majeshi ya Waislamu?!”, “Tufungulieni mipaka!”**. Kwa hakika, suluhisho linaanza kwa majeshi ya Kiislamu kusonga, kuwaondoa watawala wasaliti, na kurudisha pigo la pili kwa umbile la Kiyahudi baada ya kupata pigo la kwanza kutoka kwa watu wa Gaza. Hatua hiyo inaweza tu kufanikiwa kwa kuvunja milango ya jela la Sykes-Picot na kufuta mipaka baina ya nchi za Kiislamu ili wote waende kuinusuru ardhi iliyobarikiwa ya Palestina, na hili ni jambo ambalo majeshi pekee katika nchi za Kiislamu yanaweza kufanya, kwa sababu wao ndio watu wenye nguvu na ulinzi. Hao ndio watu halisi wa Nusrah.

Kwa hakika, kusimamisha Khilafah ni hitajio la dharura kwa Umma wa Kiislamu, linaweza kufikiwa tu na majeshi ya Kiislamu, kwani wao wana uwezo wa kuinusuru Gaza na pia wana uwezo wa kusimamisha Khilafah. Kwa hiyo, fanyeni haraka kwa ajili ya kazi nzito mara moja ya kusimamisha Khilafah Rashida ya pili kwa njia ya Utume.

Mwenyezi Mungu (swt) anasema:

وَعَدَ اللهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُم فِي الأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَى لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْناً يَعْبُدُونَنِي لا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئاً وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ

**“Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walio amini miongoni mwenu na wakatenda mema, ya kwamba atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyo wafanya makhalifa wa kabla yao, na kwa yakini atawasimamishia Dini yao aliyo wapendelea, na atawabadilishia amani baada ya khofu yao. Wawe wananiabudu Mimi, wala wasinishirikishe na chochote. Na watao kufuru baada ya hayo, basi hao ndio wapotovu.”** [An-Nur: 55].

**Mhandisi Salah Eddine Adada**
**Mkurugenzi wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

**Afisi ya Habari Kitengo cha Wanawake**

حزب التحرير
HIZB UT TAHRIR

KUMB: 24/1445 | Alhamisi, 05 Sha'aban 1445 H | 15/02/2024 M


**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Watoto mjini Gaza Wanakula Chakula cha Wanyama ili Kuishi!

BBC imeripoti juu ya watu wanaoishi katika eneo lililotengwa la kaskazini mwa Gaza na wameandika kwamba watoto hukosa chakula kwa siku kadhaa. Misafara ya misaada inazidi kunyimwa vibali vya kuingia na umbile la Kiyahudi. Umoja wa Mataifa umeonya kwamba utapiamlo mkali miongoni mwa watoto wadogo kaskazini umeongezeka kwa kasi na sasa uko juu ya kikomo hatari cha 15%. Shirika la Umoja wa Mataifa la kuratibu misaada ya kibinadamu, OCHA, linasema zaidi ya nusu ya misheni za misaada kaskazini mwa Gaza zilinyimwa njia ya kuingia mwezi uliopita na kwamba kuna ongezeko la uingiliwaji na majeshi ya Kiyahudi katika jinsi na wapi misaada inatolewa.

Baadhi ya wakaazi wameamua kusaga chakula cha mifugo kuwa unga ili kuishi, lakini hata akiba ya nafaka hizo sasa inapungua, wanasema. Watu pia wameelezea kuchimba kwenye mchanga ili kupata mabomba ya maji ya kunywa na kuoga.

Takriban watu 300,000 wanaripotiwa kuishi katika maeneo ya kaskazini mwa Gaza, na wanakaribia kukatiwa kabisa msaada. Matokeo yake, sasa kuna hatari ya njaa inayoongezeka.

Mfanyikazi mmoja wa kituo cha msaada wa matibabu, Mahmoud Shalabi huko Beit Lahia, alisema watu wamekuwa wakisaga nafaka zinazotumika kwa chakula cha mifugo kuwa unga, lakini hata hiyo sasa zinaisha alisema; "Watu hawazipati sokoni. Hazipatikani siku hizi kaskazini mwa Gaza na Mji wa Gaza. Tulichokuwa nacho ni kutoka kwa siku sita au saba za usitishaji vita [mnamo Novemba], na msaada wowote ulioruhusiwa kaskazini mwa Gaza kufikia sasa watu washautumia. Kile watu wanachokula hivi sasa ni wali, na wali pekee."

Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) liliifahamisha BBC kwamba vikosi vya jeshi la Kiyahudi vimesimamisha misafara minne kati ya mitano ya mwisho ya misaada kuelekea kaskazini, na kusababisha pengo la wiki mbili kati ya usafirishaji hadi Mji wa Gaza. Katika kitendo cha utaratibu wa uongo na propaganda msemaji wa shirika la kijeshi la Kiyahudi lililopewa jukumu la kuratibu upatikanaji wa misaada huko Gaza alisema katika mkutano wa mwezi uliopita kwamba "hakuna njaa mjini Gaza. Kwisha." Shirika hilo, Cogat, limesema mara kwa mara haliwekei kikomo misaada ya kibinadamu inayotumwa Gaza.

Tunajua kwamba ukweli mkali na uhalisia wa kutisha wa hali ya Gaza unafichwa na vyanzo vya habari uwanjani vinathibitisha vyenginevyo.

Watoto wetu wapendwa, safi, wa Gaza wanawezaje kutendewa kama wanyama kwa namna hii! Kwa hakika, watawala wa nchi za Kiislamu lazima wawajibike kwa usaidizi wao katika jinai hizi kwani wanayazuia majeshi ya Waislamu. Sisi kama Umma wa Kiislamu hatuwezi kamwe kuukubali uovu unaojitokeza unaotolewa kwa jina la ulinzi feki na uhuru wa kupambana na Mwenyezi Mungu (swt). Enyi Umma wa Kiislamu, tangazeni ukimya wa tawala hizi na mujitenge na historia inayoandikwa katika kuendeleza mipango ya Shetani. Ili Mwenyezi Mungu aturehemu Siku ya Kiyama kutokana na adhabu yake kali.

أَلَيْسَ اللَّهُ بِكَافٍ عَبْدَهُ وَيُخَوِّفُونَكَ بِالَّذِينَ مِن دُونِهِ وَمَن يُضْلِلِ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِنْ هَادٍ * وَمَن يَهْدِ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِن مُّضِلٍّ أَلَيْسَ اللَّهُ بِعَزِيزٍ ذِي انتِقَامٍ * وَلَئِن سَأَلْتَهُم مَّنْ خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ لَيَقُولُنَّ اللَّهُ قُلْ أَفَرَأَيْتُم مَّا تَدْعُونَ مِن دُونِ اللَّهِ إِنْ أَرَادَنِيَ اللَّهُ بِضُرٍّ هَلْ هُنَّ كَاشِفَاتُ ضُرِّهِ أَوْ أَرَادَنِي بِرَحْمَةٍ هَلْ هُنَّ مُمْسِكَاتُ رَحْمَتِهِ قُلْ حَسْبِيَ اللَّهُ عَلَيْهِ يَتَوَكَّلُ الْمُتَوَكِّلُونَ * قُلْ يَا قَوْمِ اعْمَلُوا عَلَى مَكَانَتِكُمْ إِنِّي عَامِلٌ فَسَوْفَ تَعْلَمُونَ * مَن يَأْتِيهِ عَذَابٌ يُخْزِيهِ وَيَحِلُّ عَلَيْهِ عَذَابٌ مُّقِيمٌ

**"Je! Mwenyezi Mungu si wa kumtosheleza mja wake? Na ati wanakutishia kwa hao wenginewe wasio kuwa Yeye! Na aliye hukumiwa na Mwenyezi Mungu kupotea hana wa kumwongoa. Na ambaye Mwenyezi Mungu anamwongoa hana wa kumpotoa. Je! Mwenyezi Mungu si Mwenye nguvu anaye weza kulipiza? Na ukiwauliza: Ni nani aliye ziumba mbingu na ardhi. Bila ya shaka watasema: Mwenyezi Mungu. Sema: Je! Mnawaonaje wale mnao waomba badala ya Mwenyezi Mungu, ikiwa Mwenyezi Mungu akitaka kunidhuru, wao wanaweza kuniondolea dhara yake? Au akitaka kunirehemu, je, wao wanaweza kuzuia rehema yake? Sema: Mwenyezi Mungu ananitosheleza. Kwake Yeye wategemee wanao tegemea. Enyi watu wangu! Fanyeni mwezavyo, mimi pia nafanya. Basi mtakuja ona. Ni nani itakaye mfikia adhabu ya kumhizi, na itakaye mshukia adhabu ya daima."** [Az-Zumar: 36-40]


**Kitengo cha Wanawake**
**katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Kuporomoka kwa Lazima Kulikokaribia



Mfalme Abdullah II wa Jordan hivi majuzi alitembelea Ikulu ya White House kupokea maelekezo kuhusu dori yake katika mauaji ya halaiki yanayoendelea Gaza. Biden alikuwa makini kuushirikisha utawala wa Jordan katika mipango yake ya kusuluhisha usitishaji vita kati ya umbile la Kizayuni na Hamas. Amejitolea kufikia makubaliano. "Mambo muhimu ya mpango huo yapo mezani," Biden alisema pamoja na mfalme, ingawa "kuna mapungufu yanayosalia." Alisema Marekani itafanya "kila linalowezekana" kuyafanya makubaliano yafanyike ikiwa ni pamoja na kusitisha mapigano kwa angalau wiki sita na kuachiliwa kwa mateka waliosalia wanaoshikiliwa na Hamas. Vile vile alisisitiza umuhimu wa Mamlaka ya Palestina katika kuchukua majukumu huko Gaza endapo Hamas haipo tena madarakani, na kusema, "lazima wajiandae kujenga dola inayokubali amani, isiyohifadhi makundi ya kigaidi kama Hamas na Jihad ya Kiislamu. ”

Hii ilifuatia raundi ya mikutano pamoja na wanasiasa wa Marekani akiwemo Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani Blinken, Waziri wa Ulinzi Austin, na Mshauri wa Usalama wa Kitaifa, ambao wamekuwa wageni wa mara kwa mara katika Mashariki ya Kati, na kusisitiza uungaji mkono wao mkubwa wa kijeshi kwa umbile la Kizayuni. Ziara hizi pia zilitoa shinikizo la kisiasa kwa viongozi wa mrengo wa kulia katika serikali ya Netanyahu kuafikiana na malengo ya Marekani ya suluhisho la dola mbili.

Kupuuza huku kwa wazi kwa Marekani kwa Ummah ni jambo ambalo halifichiki tena. Imeianika wazi Marekani mbele ya ulimwengu. Kiburi na uchokozi usio na kifani unaoonyeshwa katika kuunga mkono ugaidi na mauaji ya halaiki huku wakidai kuwezesha mazungumzo ya amani ni unafiki ambao ulimwengu unashuhudia na kuona. Misimamo hii inaweka shinikizo kubwa kwa vibaraka wanaoning'inia katika guo la Magharibi.

Suala sio tena kwamba utawala wa Jordan unashiriki katika mapambano ya kubakia hai kwake, ambayo ni dhahiri katika ushirikiano wake na Marekani na Uingereza na mikutano yao ya mara kwa mara. Hii inasisitiza hofu yao na kuyumba kwa tawala zao. Utawala wa Jordan unaamini kimakosa kwamba ushirikiano wake na umbile la Kizayuni na nchi za Magharibi unaweza kuzuia kuanguka kwake kunakokaribia.

Ummah mzima unalaani misimamo mibaya inayochukuliwa na Marekani na kutochukua hatua kwa utawala wa Jordan. Unatafuta kutoroka kutoka kwa viongozi wao na mfumo mbovu wa kilimwengu. Mabadiliko ya kweli yanaweza kupatikana tu kupitia kuanguka kwa vibaraka na vyombo vya kisiasa vya Magharibi na kukumbatia kwa kina mfumo wa Kiislamu, kupitia kusimamishwa tena kwa Khilafah ambayo itaweka ukombozi wa Palestina kama kipaumbele na kusambaratisha mtandao wa vibaraka na serikali zinazokalia ulimwengu wa Kiislamu.

مَثَلُ الَّذِينَ اتَّخَذُوا مِنْ دُونِ اللهِ أَوْلِيَاءَ كَمَثَلِ الْعَنكَبُوتِ اتَّخَذَتْ بَيْتًا وَإِنَّ أَوْهَنَ الْبُيُوتِ لَبَيْتُ الْعَنْكَبُوتِ لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ

**“Mfano wa walio wafanya walinzi badala ya Mwenyezi Mungu, ni mfano wa buibui alivyo jitandia nyumba. Na hakika nyumba dhaifu mno kuliko zote ni jumba la buibui, laiti kuwa wanajua.”** [Al-'Ankabut: 41]

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Haitham Ibn Thbait**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb utTahrir Amerika**

JIBU LA SWALI

# Uchaguzi wa Pakistan



**Swali:**

Shirika la habari la Reuters liliripoti mnamo tarehe 19 Februari 2024, "Vyama viwili vikuu vya Pakistan vinatazamiwa kukutana mnamo Jumatatu ili kujaribu kutatua tofauti za kuunda serikali ya mseto ya wachache baada ya uchaguzi ambao haukukamilika, afisa mmoja wa ngazi ya juu wa chama alisema, akisisitiza kukosekana kwa utulivu wa kisiasa na kiuchumi ... Mazungumzo ya Jumatatu itakuwa raundi ya tano kama hii baada ya Waziri Mkuu wa zamani Shehbaz Sharif kuteuliwa na chama chake cha Pakistan Muslim League-Nawaz (PML-N) kuiongoza tena nchi hiyo." (Chanzo) Uchaguzi wa Pakistan ulifanyika mnamo tarehe 8 Februari 2024, baada ya kuakhirishwa. Je, mikutano hiyo ya Jumatatu iliyotajwa ilimaanisha kutengwa kwa watu huru watiifu kwa Pakistan Tehreek-e-Insaf (PTI) kutoka mamlakani? Je, tuhma za ulaghai na udanganyifu katika uchaguzi ni za kweli? Je, mambo yanaelekea wapi baada ya uchaguzi nchini Pakistan?

**Jibu:**

Uchaguzi huo ulifanyika nchini Pakistan baada ya kuakhirishwa kwa miezi kadhaa. Samaa TV iliripoti mnamo tarehe 11 Februari 2024 “Kulingana na matokeo yaliyotangazwa hadi sasa, wagombea huru wamefanikiwa kushinda viti 101. Inafaa kutaja kwamba kati ya wagombea hao huru 101, 92 wanaungwa mkono na Pakistan Tehreek-e-Insaf huku tisa wakiwa wagombea huru. PML-N iko katika nafasi ya pili ikiwa na viti 75, huku PPP ikishinda viti 54. (Chanzo). Chaguzi hizi zilikusudiwa kuongoza nchi kuelekea utulivu wa kisiasa. Hii ni baada ya kipindi kigumu cha machafuko yaliyofuatia hoja ya Bunge ya kutokuwa na imani dhidi ya serikali ya Imran Khan mnamo 9 Aprili 2022 na kupinduliwa kwake. Kisha, Shehbaz Sharif, kaka yake Nawaz Sharif, akashika wadhifa wa Waziri Mkuu nchini Pakistan kwa niaba ya Pakistan Muslim League-Nawaz. Baada ya hapo, maandamano ya vurugu yalizuka nchini humo... Kuhusu wapi mambo yanaelekea sasa, baada ya uchaguzi nchini Pakistan, mambo yafuatayo lazima yazingatiwe:

1- Pakistan ni moja ya nchi muhimu za Kiislamu. Idadi yake kubwa ya watu milioni 250 inaifanya kuwa hifadhi kubwa ya binadamu, ili kugeuza gurudumu la uchumi na kutoa rasilimali watu kwa jeshi. Pakistan ni mojawapo ya nchi za kipekee duniani katika upande wa rasilimali watu na nguvu za kijeshi, na pia kuwa katika eneo la kimkakati.

2- Leo hii, Pakistan inachukuliwa kuwa moja ya nchi masikini duniani. Hii ni licha ya wingi wa tambarare za kilimo yenye rutuba na maji. Hii ni licha ya uwezo wake wa viwanda. Hii ni licha ya rasilimali watu kuweza kuendesha uchumi mkubwa zaidi duniani. Hii yote ni kutokana na sera zilizofeli ambazo Marekani inazisukuma, ufisadi wa kifedha na kiutawala, na kuenea kwa ugonjwa wa kutegemea wengine, kama vile China au Marekani. Hii inazuia jaribio lolote la maendeleo ya kiuchumi. Nchi hii iliteseka kutoka na mafuriko makubwa mnamo 2022 ambayo yaliharibu ardhi ya kilimo. Kisha, serikali haikuweza kutoa masuluhisho yoyote ya thamani. Mbali na kufeli kwa uchumi, kuna kutofaulu kabisa katika nyanja zote nchini Pakistan, kufeli kukuu zaidi kukiwa katika utawala, kwa muda wa miongo kadhaa.

3- Ari ya Kiislamu ya jihad ililipuka nchini Pakistan kwa namna ambayo ilizua hofu duniani kote. Hii ilitokana na athari za kadhia ya Kashmir, na vile vile athari ya uvamizi wa Kisovieti wa Afghanistan, ikifuatiwa na uvamizi wa Marekani wa Afghanistan. Matukio mengi kwa miongo

***Endelea... UK 10***

kadhaa yamefichua ari thabiti ya mapigano, ambayo imekita mizizi katika Aqida (itikadi) ya Kiislamu ya watu wa Pakistan. Kulikuwa na harakati nyingi za jihad za Kiislamu kukomboa Kashmir na Afghanistan. Kulikuwa na wito wa kuwaunga mkono Waislamu duniani kote. Harakati za kile ambacho Wamagharibi wanakiita Uislamu wa kisiasa zilikita mizizi nchini Pakistan, inayojulikana zaidi ikiwa ni ulinganizi wa kusimamisha Khilafah... Kutokana na hayo yote, mlipuko wa Uislamu nchini Pakistani umeifanya Pakistan, pamoja na Afghanistan jirani, kituo cha pili cha mvuto wa kisiasa wa Kiislamu, baada ya Mashariki ya Kati.

4- Jeshi la Pakistan linachukuliwa kuwa jeshi kubwa la kuzingatiwa, lililo na silaha hatari na uwezo wa nyuklia. Kwa sababu ya historia ndefu ya mzozo na India, Marekani inalisukuma Jeshi la Pakistan kuelekea vita vya wenyewe kwa wenyewe ndani ya Pakistan. Inalisukuma Jeshi la Pakistan kugombana na kuzozana na vuguvugu la Taliban, ambalo liliregea madarakani mwaka wa 2021, nchini Afghanistan. Marekani pia inalisukuma Jeshi la Pakistan kuelekea mpaka wa Iran. Haya yote ni ili kuiwezesha India kushiriki katika mkakati wa Marekani, kukomesha kukua kwa China, na kuishughulisha China na uwezekano wa vita na India. Kabla ya haya yote, Marekani ilikuwa imefaulu kuifanya Pakistan kuwa korido ya kufika Afghanistan, wakati wa kukaliwa kimabavu kwake kuanzia 2001-2021. Licha ya haya yote, macho ya Marekani hayaachi kuziona hatari za kimkakati kutokana na nguvu ya Jeshi la Pakistani hata kwa muda. Kwa hivyo mnamo 13 Oktoba 2022, Rais wa Marekani Biden aliita Pakistan, "mojawapo ya mataifa hatari zaidi ulimwenguni," kama ilivyoripotiwa kwenye wavuti wa Ikulu ya White House (Chanzo). Hii ni licha ya vibaraka wote wa utumishi wa kijeshi na uongozi wa kisiasa nchini Pakistan, na kuwezesha kwake sera za Marekani.

5- Kinachoongeza umuhimu wa Pakistan ni kwamba China, ambayo ni mpinzani mashuhuri wa kimataifa wa Marekani, inaitazama Pakistan kwa njia maalum. Inaisaidia Pakistan dhidi ya India. China inaipatia Pakistan silaha. China inawekeza makumi ya mabilioni ya dolari nchini Pakistan, kwa njia ya mikopo, na baadhi ya misaada, kusaidia miundombinu, barabara, bandari na viwanda. Ingawa Marekani ina udhibiti na ushawishi nchini Pakistan, inatilia shaka juhudi hizi za China, na uwekezaji nchini Pakistan.

6- Kwa kuzingatia ukweli huu, jambo la kwanza ambalo lazima lipatikane, wakati wa kuzingatia matukio ya kisiasa nchini Pakistan, ni kwamba kiongozi wa ukafiri, Marekani, amezingatia Jeshi la Pakistan na uongozi wake wa kijeshi. Ni muhimu katika utawala na ushawishi ndani ya Pakistan. Mojawapo ya matokeo makuu ya udhibiti wa Marekani juu ya Jeshi la Pakistan, na uongozi wake wa kijeshi, ni kuwekwa mbali nchi hii kutokana na migogoro, vita na India. Hii ni licha ya chokochoko za India zinazoendelea huko Kashmir, ambazo zinaongezeka mara kwa mara. Pia miongoni mwa matokeo hayo ni mkabala wa Jeshi la Pakistan katika vita vya wenyewe kwa wenyewe, na kuwasha kwake vita kaskazini-magharibi mwa Pakistan, kuwaondoa mujahidina, ambao walikuwa wakiwaunga mkono ndugu zao nchini Afghanistan wakati wa uvamizi wa Marekani wa Afghanistan. Pia miongoni mwa matokeo haya ni mapigano yanayotokea mara kwa mara na Afghanistan. Mbali na matokeo hayo, ni kwamba uvamizi wa Marekani dhidi ya Afghanistan ulikuwa unapitia katika milango ya Pakistan. Kwa hiyo, udhibiti wa Marekani juu ya uongozi wa kijeshi nchini Pakistan ndio unaoifanya Pakistan kuwa dola ambayo ni kibaraka wa Marekani.

7- Jeshi la Pakistan linadhibiti nchi kikamilifu. linaingilia kati maisha ya kisiasa, pamoja na yale ya vyama vya kisiasa, nchini. Wakati wowote mambo yanapotoka nje ya udhibiti, Jeshi la Pakistan huingilia kati kwa mapinduzi ya kijeshi, na kuwapindua watawala. Vyama viwili vya kisiasa kwa jadi vinatawala nchi, Ligi ya Waislamu wa Pakistan- Nawaz Sharif (PML-N) na Pakistan People's Party (PPP). Chama cha kwanza kinatazamwa kama chama cha mrengo wa kulia, huku chama cha pili kinachukuliwa kuwa chama cha mrengo wa kushoto. Cha kwanza kinafurahia uungwaji mkono mkubwa katika jimbo la Punjab, ilhali cha pili kinafurahia uungwaji mkono mkubwa katika jimbo la Sindh. Kuna kufeli kwa pande zote mbili katika historia. Viongozi kutoka pande zote mbili wamezama katika ufisadi, huku uongozi ukitenda kama wababe wakuu juu ya Pakistan. Hata hivyo, mbele ya kufeli huku kwa muda mrefu, na chuki kubwa ndani ya Pakistan, ambayo inawasukuma watu kuelekea kwenye harakati za kutetea Uislamu wa kisiasa, Jeshi la Pakistan liliamua kubadilisha mlingano huo. Kwa hiyo, Jeshi la Pakistan lilimleta Imran Khan, ambaye alikuwa kiongozi wa chama ambacho si kikubwa sana wakati huo, PTI, na ambaye sauti yake ilikuwa kubwa dhidi ya ufisadi. Baada ya tuhuma kuu, na kesi za kimahakama, dhidi ya Waziri Mkuu wa zamani, na kiongozi wa PML-N, Nawaz Sharif, PTI ilitawala kura za wabunge. Kwa hivyo, Imran Khan akawa Waziri Mkuu mnamo 2018.

8- Katika kipindi hicho, mahakama za Pakistan zilikuwa zikimfuatilia mtawala wa zamani Nawaz Sharif kwa mashtaka ya ufisadi. Nawaz alijiuzulu wadhifa wake mnamo Juni 2017, baada ya Mahakama ya Upeo kumtia hatiani kwa mashtaka ya ufisadi, yanayohusiana na ukwepaji kodi. Mahakama ya Upeo ilitoa hukumu kwamba Nawaz Sharif hastahili kusalia madarakani. Alihukumiwa Julai 2018 kifungo cha miaka kumi jela, kwa mashtaka ya ufisadi. Shirika la habari la Reuters liliripoti mnamo tarehe 17 Oktoba 2020 kwamba, "Waziri Mkuu wa zamani wa Pakistan Nawaz Sharif mnamo Jumamosi alimtuhumu mkuu wa jeshi la nchi Jenerali Qamar Javed Bajwa kwa kupindua serikali yake, kushinikiza mahakama, na kuipandikiza serikali ya sasa ya Waziri Mkuu Imran Khan katika uchaguzi wa 2018." (Chanzo). Haya yote, kupinduliwa kwa Nawaz Sharif, kushtakiwa kwake na kufanya uchaguzi, wakati akiwa bado korokoroni nchini Pakistan, kulitokana na uamuzi

***Endelea... UK 11***

wa Jeshi la Pakistan. Kumleta Imran Khan, aliye mbali na vyama viwili vya jadi nchini Pakistan, pia ilikuwa kwa uamuzi wa Jeshi la Pakistan.

9- Nawaz Sharif, ambaye alikuwa akitumikia kifungo, aliruhusiwa kusafiri kwenda Uingereza kwa madhumuni ya kiafya. Hii ilitokana na makubaliano naye kwamba angerudi, baada ya matibabu yake Pakistan, ili kukamilisha kifungo chake... Hata hivyo, baada ya Jeshi la Pakistan kumpindua Imran Khan, tulilolieleza katika swali na jibu lenye kichwa, "Marekani na Mabadiliko katika Vibaraka wake nchini Pakistan," la 5 Shawwal 1443 H, 5 Mei 2022, Jeshi la Pakistan lilianza kuondoa vikwazo vyote vya kisheria vya kuregea kwa Nawaz Sharif. Baada ya kupinduliwa kwa Imran Khan mnamo 2022, kakake Sharif, Shehbaz Sharif, aliteuliwa kuwa waziri mkuu. Haya ni pamoja na uamuzi wa mahakama ya federali ya kumuachilia huru kwa dhamana Nawaz Sharif, kabla ya kuwasili nchini. Pia ni baada ya Bunge kutoa sheria Juni 2023 kuweka muda usiozidi miaka mitano kwa mbunge wa Bunge hilo kugombea nafasi hiyo baada ya kutostahiki milele. Hili lilimruhusu Nawaz Sharif kuregea nchini na kujipendekeza mwenyewe, hivyo akaregea. Nawaz Sharif alikuja kutoka ng'ambo na kufika mbele ya mahakama katika maandalizi ya kuachiliwa kwake kwa mashtaka dhidi yake, na kushindana katika uchaguzi. Gazeti la 'The Independent' liliripoti mnamo tarehe 21 Oktoba 2023 kwamba, "Mahakama Kuu ya Islamabad mnamo siku ya Alhamisi ilimpa kinga dhidi ya kukamatwa siku chache kabla ya kuregea kwake." (Chanzo). Haya ndiyo yaliyotokea kikweli! Nawaz Sharif akawa mwanasiasa "msafi" tena. Akagombea uchaguzi na chama chake cha Pakistan Muslim League-N, huku Anwaar-ul-Haq Kakar akiwa waziri mkuu wa muda akisimamia uchaguzi. (Sharif alipata uungwaji mkono wa jeshi aliporegea Pakistan Oktoba iliyopita, baada ya Miaka minne uhamishoni jijini London. (Independent Arabia, 10/2/2024)). Kwa mujibu wa chanzo hicho hicho, (Kwa upande mwingine, inaaminika kuwa Nawaz Sharif aliregea serikalini baada ya kumaliza "dili" na jeshi ya kumregesha kwenye nafasi ya uwaziri mkuu kwa mara ya nne. Chama cha Insaf kinatuhumiwa na Al-Shaab akisema kwamba mapokezi rasmi ambayo Sharif aliyapata baada ya kuregea ni ushahidi wa kuwepo kwa maelewano kati yake na taasisi ya kijeshi.

10- Ni mafanikio sana kwa Nawaz Sharif. Ama kwa Imran Khan, leo yuko gerezani, akiwa amehukumiwa kwa makosa mengi. Kutokana na hukumu yake, Imran Khan alizuiwa kushiriki katika uchaguzi, huku chama chake, Pakistan Tehreek-e-Insaf, kilizuiwa kushiriki katika uchaguzi kama chama cha kisiasa. Kwa hivyo, inakuwa wazi jinsi meza za kisiasa zimebadilika nchini Pakistan. Leo, mwaka 2024, Jeshi la Pakistan limegeuka dhidi ya Imran Khan. Imran sasa yuko katika nafasi ile ile aliyokuwa nayo Nawaz Sharif mwaka 2018. Kuhusu Nawaz Sharif, ameregea kwenye umashuhuri, baada ya vikwazo vyote kuondolewa kwake, kama tulivyoonyesha. Pamoja na haya yote, inakuwa wazi jinsi uongozi wa Jeshi la Pakistan unavyoushawishi uchaguzi wa bunge. Inadhihirika wazi jinsi Jeshi la Pakistani linavyoendesha vyama hivyo vya kisiasa, ambavyo vinatafuta idhini yake, ili kupata mamlaka. Hii sio siri. Mkuu wa jeshi alimfunga Nawaz Sharif na kumrudisha Imran Khan... Kisha mkuu wa jeshi akamfunga Imran Khan na kumrudisha Nawaz Sharif! Kwa hivyo, wanasiasa bandia, kutoka miongoni mwa viongozi wa vyama, wanatumiwa kulingana na matakwa ya Marekani, kwa ajili ya kiti kibovu cha utawala! Kisha, pindi dori ya kiongozi kama huyo inapokwisha, ima anatupwa kando, au kuwekwa gerezani!

11- Uongozi wa kijeshi peke yake ndio hudhibiti serikali, na hivyo uchaguzi, kwa njia nyingi. Inajulikana kuwa mawasiliano na mtandao ulikatwa katika baadhi ya maeneo. Serikali ilisema kuwa hii ilikuwa kwa madhumuni ya kuzuia ghasia na machafuko, siku ya uchaguzi! Serikali pia inahodhi suala la kubainisha wilaya za uchaguzi, kulingana na sensa ya watu ambayo inaifanya. Kwa mtazamo huu inaweza kuongeza, au kupunguza, wilaya kwa kupendelea vyama maalum, ambavyo vina uzito wa uchaguzi katika wilaya hizo! Uchaguzi uliakhirishwa kutoka Agosti 2023 hadi Februari 2024, kwa kisingizio cha kupanga upya wilaya za uchaguzi, kwa kuzingatia sensa ya hivi punde ya idadi ya watu. Kwa njia hizi, viongozi wa chama, wanaochukua zamu madarakani, wote wana wajibu wa kuwa watiifu kwa Marekani, na kuitumikia Washington. Njama zimepangwa kwa yeyote atakayekengeuka kutoka kuvuta mstari wa Marekani, au kujitahidi kufanya hivyo, au kugongana na Jeshi la Pakistan, kama tulivyoona. Kesi za ufisadi zinaibuliwa dhidi yake, mpaka awe gerezani. Kwa hivyo, vyama vyote hivi vinafanya kazi chini ya mwavuli wa uongozi wa kijeshi wa jeshi. Ni uongozi ambao ni kibaraka wa Marekani. Vyama hivi vinaweza tu kushindana ndani baina yao wenyewe, ili Jeshi la Pakistan kuchagua kutoka miongoni mwao anayefaa zaidi kwa uteuzi...

12- Kisha, uongozi wa kijeshi unaruhusu kwenda mbele na nyuma, kuhusiana na matokeo ya uchaguzi, ili kuonyesha kuwa uko mbali na kudhibiti matokeo! Gazeti la 'The Independent' liliripoti mnamo tarehe 10 Februari 2024, kwamba, "waziri mkuu wa zamani Nawaz Sharif na waziri mkuu wa zamani Imran Khan walidai ushindi katika uchaguzi mkuu." (Chanzo). Chama cha PTI kinazingatia kuwa wagombeaji huru walipata viti 101, huku wengi wao wakiwa ni wafuasi wake, ambao ni idadi kubwa zaidi ya viti vinavyopatikana kwa chama chochote. Hii inakipa sifa ya kuwa chama cha kuongoza mchakato wa kuunda serikali. Hata hivyo, PML-N, inayoongozwa na Nawaz Sharif, ambayo ilipata viti 75 katika Bunge la Kitaifa, inasema kuwa ndiyo iliyoshinda uchaguzi huo. Hili linaregelewa katika taarifa ya mkuu wa jeshi kuhusu uchaguzi. Mrengo wa vyombo vya habari wa jeshi, ISPR, uliripoti kwamba mkuu wa jeshi alisema, "Taifa linahitaji mikono thabiti na mguso wa uponyaji ili kuondokana na

***Endelea... UK 12***

siasa za machafuko na ubaguzi." (Chanzo).

Hii ina maana kwamba PTI, chama cha Imran Khan, licha ya kupata idadi kubwa ya viti vya ubunge kupitia wagombea huru, viti vya wagombea huru vinaunda rasmi vile vya wagombea huru, na sio vya chama chochote cha kisiasa. Kwa hiyo, chama cha Nawaz Sharif kinasalia kuwa kile ambacho kina haki ya "kisheria" ya kuongoza mchakato wa kuunda serikali, kupitia muungano na vyama vyengine.

13- Baadhi ya viongozi walikiri kwamba wizi wa kura ulifanyika. Al-Jazeera iliripoti mnamo tarehe 17 Februari 2024 kwamba, "Afisa mmoja wa ngazi ya juu nchini Pakistan amesema alisaidia kuvuruga uchaguzi wa Pakistan, wiki moja baada ya kura za maoni zilizokumbwa na madai ya udanganyifu hazijaleta mshindi wa wazi ... "Tulibadilisha walioshindwa na kuwa washindi, na kuregesha kiwango cha kura 70,000 katika viti 13 vya bunge," aliwaambia waandishi... Kulingana na gazeti la 'Dawn News' la Pakistan, kamishna huyo alikiri kuwa "alihusika sana katika uhalifu mkubwa kama vile wizi mkubwa wa kura za 2024." Wakati huo huo, tume ya uchaguzi ya Pakistan ilikataa madai ya Chattha, lakini ilisema katika taarifa kwamba "itafanya uchunguzi". Katika taarifa ya habari, shirika la kusimamia uchaguzi pia lilisema hakuna afisa wake aliyewahi kutoa maagizo yoyote kwa Chattha kwa "mabadiliko ya matokeo ya uchaguzi". (Chanzo). Licha ya hayo yote, mkuu wa majeshi, baada ya kumwachilia huru Nawaz Sharif kutoka gerezani, na kumruhusu kugombea uongozi wa chama chake, anaonekana kumwandalia uwanja katika Afisi ya Waziri Mkuu. Shirika la habari la Reuters liliripoti, mnamo tarehe 19 Februari 2024, kwamba, "Vyama viwili vikuu vya Pakistan vinatazamiwa kukutana Jumatatu ili kujaribu kutatua tofauti za kuunda serikali ya mseto ya wachache baada ya uchaguzi ambao haukukamilika, afisa wa juu wa chama alisema, akisisitiza kukosekana kwa utulivu wa kisiasa na kiuchumi... Mazungumzo ya Jumatatu yatakuwa ya raundi ya tano... Chama cha Pakistan Peoples Party (PPP) cha waziri wa zamani wa mambo ya nje Bilawal Bhutto Zardari kimetangaza kuunga mkono kwa masharti PML-N, kikisema kitampigia kura Sharif kuunda serikali, lakini hakitachukua nyadhifa katika baraza la mawaziri... Serikali mpya inaweza pia kukabiliwa na mvutano zaidi wa kisiasa, huku wabunge huru wakiungwa mkono na waziri mkuu wa zamani Imran Khan aliyefungwa jela, na kuunda kundi kubwa zaidi katika bunge." (Chanzo). Kwa hivyo, uongozi wa kijeshi unamfanya yeyote unayemtaka kuwa mshindi leo, na kumfanya kuwa mshindwa na mfungwa kesho... na kadhalika! Amesema Mwenyezi Mungu (swt):

أَلَا سَاءَ مَا يَحْكُمُون

**"Tazama uovu wa wanavyohukumu!"** [Surah An-Nahl 16:59].

14- Ama kuhusu ujanja huu wa kina wa serikali ya Pakistan, na uongozi wa kijeshi kibaraka wa Marekani, ambapo kuna hali ya machafuko ya kisiasa, ambayo yanaweza kuendelea na kudhoofisha uthabiti wa nchi ... yote haya lazima yawe motisha kubwa, kwa watu wenye ikhlasi katika Jeshi la Pakistan, na nchini Pakistan kwa jumla, kuinuka na kukomesha utiifu wa nchi hiyo kwa Marekani... hii ni kwa kusimamisha tu utawala wa Mwenyezi Mungu, Khilafah Rashida. Khilafah ni ahadi ya Mwenyezi Mungu (swt). Amesema Mwenyezi Mungu (swt):

وَعَدَ اللهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ

**"Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walio amini miongoni mwenu na wakatenda mema, ya kwamba atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyo wafanya makhalifa wa kabla yao."** [Surah An-Nur 24:55]. Khilafah iko ndani ya bishara njema ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw), kuhusu kurudi kwake baada ya utawala wa kutenza nguvu ambao tuko chini yake. Hudhayfah (ra) amesema kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema,

ثُمَّ تَكُونُ مُلْكاً جَبْرِيَّةً فَتَكُونُ مَا شَاءَ اللهُ أَنْ تَكُونَ ثُمَّ يَرْفَعُهَا إِذَا شَاءَ أَنْ يَرْفَعَهَا ثُمَّ تَكُونُ خِلَافَةً عَلَى مِنْهَاجِ النُّبُوَّةِ ثُمَّ سَكَتَ

**"'Kisha utakuwepo utawala wa kutenza nguvu, utakuwepo kwa muda apendao Mwenyezi Mungu uwepo kisha atauondoa apendapo kuuondoa. Kisha itakuwepo Khilafah kwa Njia ya Utume.' Kisha akanyamaza."** Imesimuliwa na Ahmad. Utekelezaji faradhi hii kubwa unatarajiwa kutoka kwa watu wa Umma wa Kiislamu, kwa mapana na marefu… hususan kwa kuwa Pakistan iliasisiwa kwa msingi wa Uislamu kuanzia siku ya kuunda kwake, na watu wake pamoja na jeshi lake wanapenda Uislamu na Waislamu.

Muunganisho wa watawala wa Pakistan, na uongozi wake wa kijeshi, na Marekani ni rahisi kwa Mwenyezi Mungu (swt) kuubadilisha, kuliko ilivyo kwao kubadilisha mapenzi ya Ummah kwa Uislamu wake. Hivyo basi, matokeo ni kwa wachamungu ikiwa wana ikhlasi, wakafanya kazi kwa bidii, na wakajitahidi kumnusuru Mwenyezi Mungu (swt), kwani Mwenyezi Mungu (swt) ndiye msaidizi wao. Amesema Mwenyezi Mungu (swt):

وَسَيَعْلَمُ الَّذِينَ ظَلَمُوا أَيَّ مُنْقَلَبٍ يَنْقَلِبُونَ

**"Na wanao dhulumu watakuja jua mgeuko gani watakao geuka."** [Ash-Shu'ara 26:227].

**10 Sha'aban 1445 H**

**20 Februari 2024 M**